JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**OFISI YA MSAJILI WA VYAMA VYA SIASA**

Anwani ya simu: 'SIASA'
Simu: 026 2137232
Fax: 026 2136924
Tovuti: www.orpp.go.tz

Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa
Viwanja Vya Nanenane Nzuguni
Jengo la Wizara ya Kazi,
Mtaa wa Nzuguni A
P.O. Box 2851
**DODOMA**

## TAARIFA KWA UMMA

## KUKARIBISHA MAONI YA KUFANYIWA KAZI NA KIKOSI KAZI CHA MHESHIMIWA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

Tarehe 15, 16 na 17 Desemba 2021 Dodoma, kulifanyika mkutano wa wadau wa demokrasia ya vyama vingi vya siasa nchini. Mkutano huo ulifunguliwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kufungwa na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Washiriki wa mkutano huo walipendekeza na Serikali ikaridhia kwamba, kiundwe Kikosi Kazi ambacho kitachambua maoni na mapendekezo yaliyojitokeza na kuandaa mapendekezo mahususi ambayo yatawasilishwa Serikalini kwa ajili ya kufanyiwa kazi.

Tarehe 23 Desemba 2021 Kikosi Kazi hicho kiliundwa na kilizinduliwa tarehe 10 Januari 2022 na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Kikosi Kazi kilianza kazi tarehe 11 Januari 2022 na kinaendelea na kazi.

Baada ya kuchambua maoni na mapendelezo ya washiriki wa mkutano huo, Kikosi Kazi kimeainisha masuala makuu ya kufanyiwa kazi yafuatayo:-

| Na. | Suala |
|---|---|
| 1. | Mikutano ya hadhara na ndani ya Vyama vya Siasa |
| 2. | Masuala yanayohusu uchaguzi |
| 3. | Mfumo wa maridhiano ili kudumisha haki, amani, utulivu na Umoja wa kitaifa |

| | |
|---|---|
| 4. | Ushiriki wa Wanawake na Makundi Maalumu katika siasa na Demokrasia ya Vyama Vingi vya Siasa |
| 5. | Elimu ya Uraia |
| 6. | Rushwa na Maadili katika siasa na uchaguzi |
| 7. | Ruzuku ya Serikali kwa Vyama vya Siasa |
| 8. | Uhusiano wa Siasa na Mawasiliano kwa Umma |
| 9. | Katiba Mpya |

Hivyo, Kikosi Kazi kinaalika taasisi, kikundi cha watu na mtu yeyote mwenye maoni, mapendekezo au nyaraka kuhusu masuala hayo tisa au mengine yoyote yanayohusu demokrasia ya vyama vingi vya siasa, ambayo anaona yatasaidia Kikosi Kazi kuandaa mapendekezo mazuri na yanayotekelezeka, awasilishe maoni, mapendekezo au nyaraka hizo kwa njia zifuatazo:-

1. Barua pepe, taskforcemaoni@orpp.go.tz
2. WhatsApp, ujumbe kwenda kwa Katibu wa Kikosi Kazi, 0784 394883;
3. Sanduku la Posta, 2851 Dodoma; au
4. Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa iliyopo:-
    i. Dodoma, viwanja vya Nanenane Nzuguni, katika Jengo la Wizara ya Kazi, Mtaa wa Nzuguni A;
    ii. Dar-es Salaam, mtaa wa Shaaban Robert mkabala na Shule ya Msingi Bunge; na
    iii. Zanzibar, Mbweni Matrekta.

Pia Kikosi Kazi kinaandaa utaratibu wa kukaribisha taasisi, vikundi na watu maalum kuzungumza nao, ili kupata ufafanuzi wa maoni na mapendekezo yao. Ili Kikosi Kazi kiweze kutekeleza kazi zake kwa mujibu wa Mpango Kazi uliopo, mnaombwa kuwasilisha maoni, mapendekezo au nyaraka hizo, ndani ya muda wa siku thelathini na moja (31) kuanzia tarehe ya leo 14 Aprili 2022.

Karibuni sana.

Sisty L. Nyahoza
**KATIBU WA KIKOSI KAZI**

14 Aprili 2022